

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Barabara ya Kilimatinde Cheyo,  
S.L.P. 1020,  
45112 TABORA,  
Barua Pepe: [rbctabora@pccb.go.tz](mailto:rbctabora@pccb.go.tz).  
TANZANIA.  
[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TABORA – 08 JUNI, 2020**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MWENYEKITI NA MTENDAJI WA KIJJI KUFUNGULIWA KESI KWA  
MAKOSA YA RUSHWA**

TAKUKURU Mkoa wa Tabora Juni 8, 2020 inatarajia kuwafikisha mahakamani Mwenyekiti na Mtendaji wa Kijiji cha Majororo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya Rushwa.

Watuhumiwa hao wanakabiliwa na tuhuma za kuomba na kupokea hongo kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2007.

Taarifa iliypokelewa na ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Sikonge ilieleza kuwa mwezi Februari 2020 watuhumiwa waliomba hongo ya shilingi 810,000/= kutoka kwa mtoa taarifa (jina limehifadhiwa) ili waweze kumuachia huru na kumfutia makosa ya kuishi na mwizi nyumbani kwake bila kutoa taarifa katika Serikali ya Kijiji. Baada ya taarifa kupokelewa uchunguzi ulifanyika na kuthibitisha pasi na shaka kuwa watuhumiwa hao walijihusisha na makosa hayo hivyo watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

**PIA KATIKA HATUA NYINGINE, TAKUKURU** Mkoa wa TABORA inategemea kumfikisha mahakamani Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwitikio Katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na11/2007.

Mtuhumiwa anakabiliwa na tuhuma hizo baada ya kujipatia shilingi 200,000/- kutoka kwa mwananchi kwa lengo la kumsadia kwenye kesi yake iliyokuwa ikimkabili katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji.

## **WITO**

TAKUKURU mkoa wa TABORA inawakumbusha wananchi wote na hasa watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinavyoelekeza na kuhakikisha wanawahudumia wananchi bila upendeleo na kuepuka kujihusisha na vitendo vya Rushwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Tunaelekea kwenye uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais, naomba nichukue nafasi hii kuwakumbusha wanaotegemea kugombea nafasi za uongozi katika mkoa wetu kutojihusisha na vitendo vya rushwa na kuwarubuni wapiga kura, vilevile wapiga kura tusikubali kurubuniwa kwa rushwa ya aina yeyote. TAKURU Mkoa wa Tabora tumejipanga na yeyote atakayethubutu kujihusisha na vitendo vya rushwa hatabaki salama.

TAKUKURU haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaothibitika kujihusisha na vitendo vya Rushwa katika kutekeleza majukumu yao.

Tunatoa Shukrani kwa wananchi na vyombo vya habari kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa kuendelea kutoa taarifa ya vitendo vya Rushwa na kueleimishana jamii juu ya athari za Rushwa.

## **ASANTENI**

**Imetolewa Na**

MUSA O. CHAULO

**MKUU WA TAKUKURU (M) TABORA**